Karatasi hii imetokana na kijitabu cha ***Ujuzi wa kuajiliwa na utamaduni wa maeneo ya kazi nchini Australia***. Imeandikwa kwa makusudi katika Kiingereza chepesi sana kusaidia wahamiaji ambao bado wanakuza uwezo wao wa Kiingereza

Habari hizi zinapatikana kwa kuombwa katika mifumo tofauti kama Breli, kanda iliyorekodiwa na diski ya kompyuta.

Kwa habari zaidi tembelea trainingwa.wa.gov.au

Government of **Western Australia**
Department of **Training**
and Workforce Development

Waajiri wanathamini wafanyakazi wanaojiongoza wenyewe.

Sio vizuri kuchelewa. Kila mara uwahi kufanya mambo. Uwahi kufika kazini na hudhuria mikutano kwa muda.

Kama utakawia kazini, piga simu au tuma ujumbe kwa mwajili au meneja wako.

Omba radhi, eleza sababu na sema utafika lini.

Waajiri wanathamini wafanyakazi wanaoendelea kujifunza ujuzi mpya.

Watu wanaofanya kazi nchini Australia wanatazamiwa kuendeleza ujuzi wao wa kazi muda wote.

Kila mara jaribu kupiga hatua jinsi unavyofanya kazi na kuboresha ujuzi wako wa kazi.

Wakati mwingine unatakiwa kuhudhuria kozi ya masomo nje ya kazi.

Wakati mwingine, unaweza kujifunza kitu kipya kazini. Uliza meneja wako au mwajiri wako kuhusu hili.

Ni muhimu kufanya kazi kwa bidii kuimarisha ujuzi wako.

Waajiri wanathamini wafanyakazi wanaoelewa teknolojia- mashine, vifaa na ufundi.

Mazingira ya kazi yanatumia teknolojia- mashine, vifaa na ufundi- kuumba au kufanya vitu kazini. Kwa mfano:

- mashine ya kuhesabu pesa, mashine ya kahawa;
- kompyuta, printa na mashine ya kutoa vivuli; na
- magari, winchi na vyenzo za kuinua.

Mara nyingi, kazini utafundishwa jinsi ya kutumia mashine hizi.

Mara nyingine, unahitaji kujua jinsi ya kutumia teknolojia kabla ya kupata kazi. Matangazo mengi ya kazi yanaeleza hili.

Kumbuka, sio kwamba mazingira yote ya kazi hapa Australia yanafanana.

Hivyo, kama huna uhakika, tazama, sikiliza na uliza.

Mwongozo kwa wahamiaji

wanaotaka kuingia maeneo ya kazi ya Australia ya Magharibi

Maeneo ya kazi ya Australia yako tofauti na maeneo ya kazi ya nchi zingine nyingi.

Mwongozo huu unaelezea jinsi tunavyofanya vitu katika maeneo ya kazi hapa Australia. Ni matumaini yetu itakusaidia kujiandaa kwa kazi hapa Australia ya Magharibi.

Kitu cha muhimu sana kukumbuka ni:

Kama huna uhakika, tazama, sikiliza na uliza.

TRAINING WA
Careers. Skills. Opportunities.

Kiingereza ni lugha ya mawasiliano yote katika maeneo ya kazi nchini Australia.

Ni lazima ujifunze kusoma, kuandika na kusema Kiingereza kidogo ili kufanya kazi vizuri katika Australia.

Hii itakusaidia:

- elewa na fuatilia maelekezo ya mdomo;
- soma na fuatilia alama za usalama na maelekezo;
- andika maneno na ujumbe;
- elewa haki na wajibu wako; na
- fanya marafiki kazini.

Maeneo mengi ya kazi hapa Australia hayaweki heshima mbele kuliko nchi zingine.

Kwa mfano, watu wengi hutumia majina ya mwanzo.
Hii mara nyingi hushangaza watu kutoka nchi zingine.
Utahitajika pengine kuchukua muda kuelewa hii.
Ni SAWA. Kumbuka:

Kama huna uhakika, tazama, sikiliza na uliza.

Waaustralia wanafupisha maneno mara nyingi-kwa mfano, wanaweza kusema "mguu" , siyo 'mpira wa mguu'. Mara nyingi wanatumia kifupi. Uliza rafiki mfanyakazi mwenzako arudie na akuelezee neno usiloelewa. Redio na televisheni vitakusaidia pia.

Waaustralia wengi wanatumia pia maneno matusi katika mazungumzo ya kawaida. Baadhi ya watu wanafikiri matusi ni mabaya, lakini Waaustralia wengi hawaumizwi na hilo. Utahitaji muda kuelewa hili. Kama ukiumizwa, mwambia anayekwambia anyamaze. Ni SAWA.

Kumbuka: kutumia matusi hakukubaliwi katika mazingira ya kawaida, kama vile mikutano au mahojiano ya kazi.

Nchini Australia, wanaume na wanawake, vijana na wazee, watu wenye ulemavu na watu kutoka nchi mbalimbali wote hufanya kazi pamoja. Hiki ni kitu cha kawaida.

Katika Australia ya Magharibi, kila mtu ana haki sawa. Mwajiri na mwajiriwa lazima waheshimu sheria kuhusu ubaguzi na usawa kwa wote.

Kwa mfano, hakuna mtu anayeweza kumbagua mtu mwingine kwa sababu ya jinsia yake, umri, asili, rangi, utamaduni, dini, ujauzito, ulemavu, hali ya ndoa, imani za kisiasa, majukumu ya familia, au mabadiliko ya kijinsia.

Unyanyasaji wa kijinsia au rangi ni kinyume cha sheria pia.

Kamishna ya Usawa kwa wote ya Australia ya Magharibi inaweza kukupa ushauri juu ya hivi.

Kila mtu lazima akuheshimu.
Lazima uheshimu kila mtu.

Ni kitu cha kawaida pia kuwa rafiki wa kila mtu.

- Tazama machoni unapokuwa ukizungumza na mtu.
- Kwa kawaida, usiguse watu wengine.
- Shika mkono sawasawa unaposalimiana na mtu kwa mara ya kwanza. Kama haujisikii kushikana mkono, tikisa kichwa na kutabasamu. Sema unajisikia vizuri kukutana na huyo mtu.

Kwa kawaida, ibada za kidini sio sehemu ya siku ya kazi. Kama unahitaji kuabudu kazini, jadiliana na mwajiri wako

Nchini Australia, waajiri wengi wana 'miongozo ya wazi'-yaani, wanahitaji waajiriwa wazungumze nao kuhusu matatizo au habari zingine za kazi. Katika Australia, hii ni kawaida.

Kumbuka:

Kama huna uhakika, tazama, sikiliza na uliza.

Waajiri wanathamini kufanya kazi katika timu. Wanapenda waajiliwa wanaoweza kushirikiana na kutumika katika timu.

Wafanyakazi wengine watakuomba kuwasaidiahasa kama kuna kitu inabidi kifanywe haraka. Waajiri wanapenda waajiriwa ambao wako tayari kusaidia kila mara.

Watu wengi watakuwa tayari kukusaidia, ukiwaomba.

Maeneo mengi ya kazi yana matukio ya kufurahisha kama vile babekiu au mlo maalumu. Hivi vinasaidia kujenga uhusiano mzuri kati kila mmoja.

Maeneo ya kazi pia husherehekea sherehe za kuzaliwa au mtu anapoondoka kazini. Kila mmoja anatoa pesa kidogo kumnunulia zawadi. Hii ni kawaida.

Kama mtu akikuomba 'kuleta sahani' kwenye tukio la kawaida leta sahani ya chakula kuchangia na kila mmoja.

Mara nyingi, kuna vinywaji vya kulevya kwenye matukio ya furuha. Ni SAWA kunywa juisi au vinywaji visivyolevya, kama unapendelea.

Waajiri wanathamini waajiriwa wanaoweza kutatua matatizo katika kazi zao za kila siku.

Kwenye siku yako ya kwanza maeneo mengi ya kazi wataelezea:

- kazi yako;
- habari za usalama na afya; na
- nani wa kuuliza msaada ukiwa na tatizo

Kama una tatizo jipya, jiulize-'naweza kulitatua mwenyewe au nahitaji msaada?'

Kama unajua unaliweza mwenyewe, litatue.

Kama huna hakika, omba msaada.

Waajiri wanathamini waajiriwa wanaofikiri jinsi ya kuifanya kazi yao vizuri.

Maeneo ya kazi Australia wanajaribu kupiga hatua kila mara.

Wanajaribu kupunguza gharama. Wanajaribu kuboresha bidhaa. Wanajaribu kuboresha huduma ya wateja.

Unaweza kuwasaidia kufanya hivi. Kwanza, jifunze kuhusu kazi yako na maeneo ya kazi. Harafu, kama una wazo la kujenga, umwambie mwajiri wako.

Waajiri wanathamini waajiriwa wanaopangia kazi zao na kuzitekeleza.

Panga kazi zako mwanzoni wa kila siku.

Kama una kazi nyingi za kufanya, fikiri kuhusu muda wako na weka malengo ya kazi ya siku. Fanya kazi ya muhimu zaidi kwanza.

Tunza nafasi yako ya kazi, vifaa vyako na karatasi zako za kazi katika utaratibu mzuri.

Fuata utaratibu na mwongozo wa maeneo yako ya kazi. Kail mara fanya kazi kwa usalama.

Kumbuka:

Kama huna uhakika, tazama, sikiliza na uliza.